



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO

MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA
CHUO CHA USAFIRI WA ANGA



MAFUNZO YA URUSHAJI WA NDEGE ZISIZOKUWA NA RUBANI



Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (Civil Aviation Training Centre) kilichopo jengo la zamani la uwanja wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) “terminal one” anawatangazia mafunzo ya ndege zisizo na rubani yaani Drones Pilot Training itakayoendeshwa kwa kushirikiana na Chuo cha Prowings Training Limited cha Afrika Kusini kuanzia tarehe 18 Januari 2021 kwa muda wa wiki nne (4).

Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne au zaidi, ajue kusoma na kuandika kiingereza na pia awe na umri kuanzia miaka 21.

Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa masaa sita (6) kila siku kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa alisiri. Mafunzo yataendeshwa kwa nadharia darasani na kwa vitendo katika viwanja vya Tanganyika packers – Kawe.

Kinadharia washiriki watajifunza kuhusu:

- Sheria za usafiri wa anga
- Uelewa wa ndege zisizokuwa na rubani
- Uwezo wa ndege, mipango na upangaji wa mizigo
- Hali mbalimbali za kiutendaji zinazoweza kuhatarisha shughuli za urushaji wa ndege zisizo na rubani

ISO 9001:2015 Certified

Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere, Jengo la Abiria Namba1, S.L.P 18157, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2844437/39/43 Namba ya Nukushi: +255 22 2844128 Barua pepe: catc@tcaa.go.tz Tovuti: www.catc.ac.tz

- Hali ya hewa
- Mifumo ya ndege zisizokuwa na rubani inayoiwezesha kupaa angani
- Taratibu na shughuli za urushaji wa ndege zisizokuwa na rubani
- Kanuni za urukaji wa ndege zisizokuwa na rubani
- Mawasiliano ya sauti kwa wana anga

Ada: 1,980,000/= ambayo itajumuisha chai ya saa nne, chakula cha mchana, vifaa vya kufundishia na gharama za usafiri kwenda viwanja vya Tanganyika packers kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

Baada ya mafunzo wahitimu watatunukiwa vyeti vitakavyowawezesha kuomba leseni ya urushaji wa ndege hizo kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

Fomu za maombi zinapatikana Chuoni au unaweza kupakua na kujaza fomu ya maombi kutoka kwenye tovuti ya Chuo cha Usafiri wa Anga www.catc.ac.tz. Nafasi ni chache, tuma maombi yako mapema na lipa ada yako ili kuwahi nafasi.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Mkuu wa Chuo, simu na: +255 715 527575, Barua pepe: aristid.kanje@tcaa.go.tz au

Mratibu wa mafunzo, simu na: +255 764 555054, Barua pepe: hamis.kisesa@tcaa.go.tz

Imetolewa na:

**Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC),
Jengo la zamani-Uwanja ndege wa kimataifa wa Mwalimu
Julius Nyerere (JNIA) Terminal one,
S.L.P. 18157,
DAR ES SALAAM.**